# KANUNI ZA KIKRISTO

## MAJIBU YA MITIHANI

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| 1. KITABU CHA MUNGU | 4 |
| 2. SIFA ZA MUNGU | 6 |
| 3. UTATU WA MUNGU | 7 |
| 4. UBINADAMU | 8 |
| 5. DHAMBI | 9 |
| 6. ROHO | 10 |
| 7. KRISTO | 12 |
| 8. WOKOVU | 13 |
| 9. MASUALA YA WOKOVU | 14 |
| 10. ROHO MTAKATIFU | 15 |
| 11. UTAKATIFU WA KIKRISTO | 16 |
| 12. KANISA | 17 |
| 13. HATIMA YA MILELE | 19 |
| 14. MATUKIO YA MWISHO | 20 |
| 15. KANUNI ZA IMANI ZA KALE | 21 |

# SOMO LA 1

## KITABU CHA MUNGU

1. Ufunuo wa Jumla Ni Nini?

   Ufunuo wa Jumla ni kile ambacho Mungu ametuonyesha kuhusu mwenyewe kupitia uumbaji wake.

2. Je, Mungu ametoa Ufunuo Maalum kwa njia gani mbili?

   - Maandiko yaliyohamasishwa
   - Yesu, mwana wake

3. Je, Ufunuo Maalum hufanya mambo gani matatu yasiyofanywa na Ufunuo wa Jumla?

   - Unaeleza kuhusu Mungu.
   - Unaeleza kuhusu Anguko na dhambi.
   - Unaonyesha njia ya kupatanishwa na Mungu.

4. Je, Biblia inatoa dai gani kujihusu?

   Ni Neno la Mungu.

5. Orodhesha sababu sita zinazotufanya tujue kwamba Biblia ni Neno la Mungu.

   - Maelfu ya taarifa za Biblia zimethibitishwa.
   - Hakuna kauli yoyote ya Biblia ambayo imekanushwa.
   - Biblia haijikanushi yenyewe.
   - Injili inathibitishwa na matokeo yake.
   - Roho wa Mungu ananena kupitia Biblia.
   - Biblia inaongoza uhusiano wetu na Mungu.

6. Je, kwa nini Biblia ni yenye faida kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki? (2 Timotheo 3:16).

   Kwa sababu ilihamasishwa na Mungu.

7. Je, Bibilia inatoa maelezo gani juu ya uhamasisho yanayotuhakikishia kwamba waandishi walizuiwa ili wasifanye makosa?

   Waliongozwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:21).

8. Orodhesha njia nne za uhamasisho ambazo Mungu alitumia.

- Sauti ya kusikika
- Ndoto
- Maono
- Kusema na maneno yakaandikwa

9. Je, inamaanisha nini kwamba Biblia ilihamasishwa?

Ni Neno la Mungu kikamilifu, hata maneno yenyewe yaliyotumiwa.

10. Je, inamaanisha nini kwamba Biblia haiwezi kuwa na makosa?

- Haiwezi kushindwa.
- Inaweza kuaminiwa.
- Kamwe haitatupotosha.

11. Je, inamaanisha nini kwamba Biblia haina makosa?

Ni sahihi katika kila kauli inayotoa.

# SOMO LA 2

## SIFA ZA MUNGU

1. Je, sifa muhimu zaidi ya mtu ni ipi?

    Dhana yake kuhusu Mungu.

2. Je, fundisho la kwanza la maandiko ni lipi?

    Mungu ndiye Muumba wa vyote vilivyopo.

3. Taja sifa ya Mungu inayolingana na kila kauli:

    - Hatuwezi kueleza jinsi Mungu anavyoonekana: *roho*
    - Mungu amekuwepo siku zote: *wa milele*
    - Mungu ana akili, hisia na nia: *mwenye nafsi*
    - Mungu ni yule yule siku zote: *habadiliki*
    - Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka: *mweza yote*
    - Mungu huona kila kitu: *yuko kila mahali*
    - Mungu alimtuma Mwanawe ili tuweze kupata rehema: *upendo*
    - Mungu ana nafsi tatu katika asili yake: *Mwenye Utatu*
    - Mungu ni mkamilifu kabisa katika maadili: *mtakatifu*
    - Mungu hajifunzi chochote: *mjua yote*
    - Matendo ya Mungu daima ni ya haki: *mwenye haki*

# SOMO LA 3

## UTATU WA MUNGU

1. Je, ulimwengu unaonyeshaje asili ya Mungu?

    Ulimwengu una vipengele vitatu - nafasi, wakati na mata.

2. Je, ni kauli gani tatu za kibiblia ambazo ni msingi wa kanuni ya Utatu wa Mungu?

    - Kuna Mungu mmoja tu.
    - Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wote ni Mungu.
    - Hawa watatu wanahusiana kati yao kama nafsi tofauti.

3. Je, mfumo wa mahusiano ndani ya Utatu wa Mungu ni upi?

    Baba ndiye kichwa, kisha Mwana, kisha Roho.

4. Je, mfumo wa familia au kanisa unalinganaje na mfumo wa Utatu wa Mungu?

    Washiriki wote wa familia au kanisa wana thamani sawa, lakini si wote wana nafasi ile ile ya mamlaka.

5. Kama watu wanaoamini Utatu wa Mungu, tunapaswa kuomba nani?

    - Kwa Baba, katika Roho, kupitia kwa Mwana
    - Kwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu

6. Taja nadharia tatu potovu za kawaida kuhusu Utatu wa Mungu.

    - Mungu kwa kweli ni mmoja lakini amechukua majukumu tofauti.
    - Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni nafsi tatu tofauti.
    - Nafsi moja katika Utatu wa Mungu ni duni kuliko nyingine.

# SOMO LA 4

## UBINADAMU

1. Kulingana na Mwanzo 1:26-27, watu ni wa kipekee kwa jinsi gani wakilinganishwa na viumbe wengine wote?

   Wameumbwa kwa mfano wa Mungu.

2. Taja sababu tatu zinazotufanya tujue kwamba mfano wa Mungu katika ubinadamu si mfano wa kimwili.

   - Mungu ni roho.
   - Kutengeneza sanamu za Mungu zinazofanana na mwanadamu ni ibada ya sanamu.
   - Watu wameumbwa kimwili kwa ajili ya maisha duniani.

3. Orodhesha vipengele saba vya mfano wa Mungu katika ubinadamu. (Vyovyote saba)

   - Silika ya ubunifu
   - Uwezo wa kufikiria
   - Uwezo wa kuwasiliana
   - Asili ya kijamii
   - Dhamiri ya kimaadili
   - Uwezo wa kuchagua
   - Kutokufa
   - Uwezo wa kupenda
   - Uwezo wa kuabudu

4. Je, tumeumbwa kwa mfano wa Mungu kwa sababu gani mbili?

   - Ili tuwe katika uhusiano na Mungu
   - Ili tumwabudu Mungu

5. Je, ni uwezo gani unatokana na dhamiri ya kimaadili?

   Uwezo wa kuelewa dhana ya mema na mabaya

6. Je, uwezo wa watu wa kufanya machaguo halisi una umuhimu gani? (Taja umuhimu wowote mmoja kati ya mawili)

   - Tunawajibika kwa Mungu.
   - Tunaweza kutubu na kuamini injili.

# SOMO LA 5

## DHAMBI

1. Orodhesha sababu tatu kwa nini ni lazima tuelewe dhambi.

    - Ili tuelewe hali ya ulimwengu
    - Ili tuelewe neema na wokovu
    - Ili tuelewe utakatifu

2. Je, tunajuaje kwamba dhambi haikuwa kosa la Mungu?

    Mungu aliumba kila kitu kikiwa kamili, bila dosari.

3. Toa ufafanuzi wa sentensi moja kwa kila moja ya yafuatayo: dhambi ya makusudi, upotovu wa kurithi, na ukiukaji usio wa makusudi.

    Dhambi ya makusudi ni ukiukaji wa makusudi wa mapenzi ya Mungu yanayojulikana.

    Upotovu wa kurithi ni upotovu wa asili ya kimaadili ya mwanadamu ambao unampa msukumo wa kutenda dhambi tangu anapozaliwa.

    Ukiukaji usio wa makusudi ni matendo yanayokiuka Neno la Mungu kwa bahati mbaya au kwa kutojua.

4. Je, ni kwa nini tunapaswa kutaka kuelewa na kutekeleza mapenzi ya Mungu vizuri zaidi?

    - Hatutaki kufanya jambo lolote lisilompendeza Mungu.
    - Kuna matokeo mabaya ya kutenda mabaya hata kama ni bila kukusudia.
    - Tunahitaji kuwa mifano bora kama Wakristo.
    - Tukijaribu kuepuka mapenzi ya Mungu tunakuwa na hatia ya dhambi.

# SOMO LA 6

## ROHO

1. Je, tunajuaje kwamba malaika kwa kawaida hawana miili ya nyama?

    Malaika ni roho.

2. Je, malaika waliumbwa wakati gani?

    Wakati fulani kabla ya uumbaji wa dunia.

3. Je, malaika hufa?

    Malaika hawafi.

4. Taja njia nne zinazotufanya tujue kuwa malaika wana nafsi.

    - Wanaweza kusema na kuwa na mazungumzo.
    - Wanamwabudu Mungu.
    - Wana hisia.
    - Wana uwezo wa kiakili.

5. Taja maneno manne yanayotumiwa katika Biblia kurejelea malaika.

    - Makerubi
    - Maserafi
    - Malaika Mkuu
    - Roho

6. Je, ni jambo gani ambalo malaika huwafanyia watu wanaomtumikia Mungu?

    Wao huwazunguka na kuwalinda.

7. Je, asili ya pepo waovu ni ipi?

    Wao ni malaika waliomuasi Mungu.

8. Je, mwabudu sanamu anaabudu nini hasa?

    Pepo / roho waovu

9. Je, hatima ya mwisho ya Shetani na pepo wengine waovu ni ipi?

    Ziwa la moto

**10.** Je, waumini wanapaswa kufanya nini ili kujilinda kutokana na mashambulizi ya kiroho?

Kuvaa silaha za kiroho (Waefeso 6:13).

# SOMO LA 7

## KRISTO

1. Je, kipaumbele cha Masihi kilikuwa kipi?

    Kuwakomboa watu kutokana na dhambi

2. Je, kanisa la awali lilimaanisha nini waliposema "Yesu ni Bwana"?

    Yeye ni Bwana wa wote, Muumba na Mungu wa ulimwengu wote.

3. Je, ni jinsi gani Yesu ni Mwana wa pekee wa Mungu?

    Yeye ndiye kiumbe pekee aliye na asili kama ya Baba kikamilifu.

4. Je, umwilisho ni nini?

    Mungu kuchukua mwili wa mwanadamu, kuwa mwanadamu.

5. Orodhesha sababu tatu zinazofanya iwe muhimu kwamba Yesu ni mwanadamu.

    - Angeweza kuteseka na kufa kama dhabihu.
    - Haki yake inaweza kutufanya tuwe wenye haki na kutupa uzima.
    - Anaweza kuwa kuhani wetu anayetuwakilisha mbele za Mungu.

6. Orodhesha sababu tatu zinazofanya iwe muhimu kwetu kujua kwamba Yesu ni Mungu.

    - Kifo chake kama dhabihu kina thamani isiyo na kikomo.
    - Ana uwezo wa kutuokoa.
    - Ni lazima tumwabudu kama tunavyomwabudu Baba.

7. Je, ni sababu gani mbili zilizofanya dhabihu ihitajike?

    - Ili Mungu atusamehe na bado awe mwenye haki na mtakatifu
    - Ili kuonyesha kwamba dhambi ni jambo zito sana

8. Je, kwa nini Yesu alikufa msalabani badala ya kufa kwa njia nyingine?

    Ilionyesha kwamba alijitwalia laana ya Mungu.

9. Orodhesha sababu tatu zinazofanya ufufuo wa Yesu kimwili uwe muhimu.

    - Ulionyesha ushindi wake kamili dhidi ya dhambi na mauti.
    - Ulithibitisha kwamba alikuwa kile alichodai kuwa.
    - Unatuhakikishia kwamba sisi pia tutafufuliwa kutoka kwa wafu.

# SOMO LA 8

## WOKOVU

1. Je, kwa nini msalaba ni chukizo kwa watu wengi?

    Msalaba unamaanisha kwamba wao ni wenye dhambi wanaohitaji msamaha.

2. Orodhesha mambo manne ambayo ni ya kweli kuhusu kila mwenye dhambi asiyetubu.

    - Kila mwenye dhambi ana hatia ya kutenda matendo mengi ya dhambi.
    - Yeye ni adui wa Mungu.
    - Amepotoka katika matamanio yake.
    - Hana uwezo wa kubadilisha hali yake.

3. Je, kwa nini msamaha bila upatanisho haumletei Mungu heshima?

    Utamfanya aonekane kuwa yeye si mwenye haki wala si mtakatifu.

4. Je, ni kwa njia gani mbili Yesu alistahili kipekee kuwa dhabihu?

    - Hakuwa na dhambi.
    - Alikuwa Mungu na mwanadamu.

5. Je, mtazamo wa mwenye dhambi anayetubu ni upi?

    - Anajiona ana hatia na anastahili adhabu.
    - Yuko tayari kucha dhambi zake.

6. Mtu akiwa na imani inayookoa, anaamini nini?

    - Hawezi kufanya lolote ili kujihesabia haki.
    - Dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake.
    - Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, akishinda dhambi na mauti.
    - Mungu anamsamehe kwa msingi wa imani pekee.

7. Je, mtu anawezaje kujua kwa uhakika kwamba ameokoka?

    - Ametubu kikweli.
    - Anatumainia ahadi za Mungu katika maandiko.
    - Amepokea ushuhuda wa Roho.

# SOMO LA 9

## MASUALA YA WOKOVU

1. Je, mojawapo ya mada kuu za 1 Yohana ni ipi?

   Hakikisho la kibinafsi la wokovu

2. Je, 1 Yohana inasisitiza zaidi sifa gani ya muumini?

   Ushindi dhidi ya dhambi

3. Je, ni mambo gani manne tunayojua kutoka katika 1 Wakorintho 10:13?

   - Majaribu huja kwa sababu ya ubinadamu wetu.
   - Mungu anajua mipaka yetu.
   - Mungu huweka mipaka katika majaribu yanayotujia.
   - Mungu hutoa kile tunachohitaji kwa ajili ya ushindi.

4. Je, muumini huendeleaje kukaa ndani ya Kristo?

   Kwa kutii amri za Kristo

5. Je, tunadumishaje uhusiano unaookoa na Kristo?

   Kwa kumwamini na kumtii Mungu

# SOMO LA 10

## ROHO MTAKATIFU

1. Orodhesha sifa tatu za mwitikio wa kanisa la awali kwa Roho Mtakatifu.

    - Walimheshimu Roho Mtakatifu katika uungu wake.
    - Walikuwa na ufahamu wa uwepo, mwongozo, na kazi ya Roho Mtakatifu.
    - Walitambua utegemezi wao kwa Roho Mtakatifu na wajibu wao wa kumwitikia.

2. Je, tunajuaje kwamba Roho Mtakatifu ana utu?

    Ana akili, nia, na hisia.

3. Orodhesha njia tano ambazo kwazo tunajua kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu.

    - Anajua mambo yote.
    - Yuko kila mahali.
    - Ana nguvu zote.
    - Anaweza kukufuriwa.
    - Yeye ni wa milele.

4. Orodhesha kazi tisa za Roho Mtakatifu.

    - Anasadikisha juu ya dhambi.
    - Anamwezesha mtu kuzaliwa upya, akimpa uzima mtu ambaye alikuwa mfu katika dhambi.
    - Anampa muumini hakikisho la kibinafsi kwamba ameokolewa.
    - Anaishi ndani ya kila muumini.
    - Anawezesha uelewa wa ukweli wa Mungu.
    - Anawaita watu kwenye huduma maalum na kuongoza maamuzi katika huduma.
    - Anamtakasa muumini, akiusafisha moyo wake ili kumfanya awe mtakatifu.
    - Anatoa uwezo wa kuishi kwa ushindi dhidi ya dhambi.
    - Anazaa matunda ya kiroho katika maisha ya muumini.
    - Anatoa karama kwa ajili ya huduma.
    - Anatoa upako maalum wa nguvu kwa ajili ya huduma.
    - Anamsaidia muumini kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu.
    - Anakuza umoja na ushirika wa kanisa.

5. Je, ni kipi kipaumbele cha juu zaidi cha Roho Mtakatifu katika kazi yake maishani mwetu?

    Kutupa ushindi dhidi ya dhambi na kutakasa mioyo yetu

# SOMO LA 11

## UTAKATIFU WA KIKRISTO

**1.** Je, ni nini maana ya msingi ya neno *takatifu*?

Kutengwa, kuwekwa wakfu kwa kusudi fulani

**2.** Je, inamaanisha nini Mungu kuwa mtakatifu?

Mungu ametengwa kabisa na kitu chochote chenye dhambi, najisi, cha kawaida au kisichofaa kwa nafsi na nafasi yake ya kiungu.

**3.** Je, kwa nini utakatifu ni muhimu kwa ibada?

- Tunampenda Mungu na tunataka kuwa kama yeye.
- Tunampenda Mungu na tunataka kumpendeza.

**4.** Je, utakatifu wa Kikristo huanza wakati gani?

Mtu anapookoka

**5.** Je, inamaanisha nini kuenenda katika nuru?

Kuendelea kumtii Mungu kadiri tunavyozidi kujifunza ukweli wake

**6.** Je, ni nini kinatokea kwa muumini wakati wa mchakato wa utakaso wa maisha yote?

Muumini anazidi kutengwa na dhambi na dunia na kujitoa zaidi kwa Mungu.

**7.** Je, upotovu wa kurithi ni nini?

Upotovu wa asili ya kimaadili ya mtu ambao unampa msukumo wa kutenda dhambi tangu anapozaliwa

**8.** Je, muumini anawezaje kukosa lawama katika mwili, nafsi na roho wakati Bwana atakaporudi?

Kwa kutakaswa kikamilifu

# SOMO LA 12

## KANISA

1. Je, enzi ya kanisa ilianza wakati gani?

    Katika siku ya Pentekoste

2. Je, kwa nini kanisa linaweza kuitwa la kitume?

    Kwa sababu mafundisho ya mitume ndio kanuni za msingi za kanisa

3. Je, vipengele vinne vya asili ya kanisa ni vipi?

    - Huduma ya Yesu
    - Wokovu uliotolewa na Kristo
    - Tukio la Siku ya Pentekoste
    - Ukuzaji wa kanuni ya kitume

4. Je, kanisa la dunia nzima ni akina nani?

    Waumini wote wa nyakati zote na mahali pote

5. Je, kanisa la kieneo ni nini?

    Jamii ya waumini katika sehemu moja ambao kwa pamoja wanafanya kazi ya mwili wa Kristo

6. Je, neno *kanisa katoliki* lilimaanisha nini hapo awali?

    Kanisa la dunia nzima linalojumuisha Wakristo wote

7. Je, kanisa la dunia nzima limeunganishwa na mambo gani mawili?

    - Kanuni za mitume
    - Uhusiano na Kristo unaobadilisha maisha

8. Je, kwa nini ni vizuri kwa kanisa kuwa na taarifa iliyoandikwa ya kanuni wanazoshiriki?

    Inaonyesha ni kanuni gani zinaunganisha kikundi hicho cha waumini kwa ajili ya ibada na huduma ya mara kwa mara yenye umoja.

9. Orodhesha makusudi sita ya kanisa la kieneo. (yoyote sita)

- Kufanya kazi ya uinjilisti
- Kuabudu kama kutaniko
- Kudumisha kanuni
- Kuwasaidia wachungaji kifedha
- Kutuma na kuwasaidia mamisionari
- Kuwasaidia washirika wenye mahitaji
- Kuwatia nidhamu washirika wanaoanguka katika dhambi
- Kutekeleza ubatizo na Meza ya Bwana
- Kuwafunza waumini hadi wafikie ukomavu
- Kuhudumia mahitaji ya jamii

# SOMO LA 13

## HATIMA YA MILELE

1. Je, shughuli kuu ya mbinguni ni ipi?

    Ibada

2. Orodhesha vitu vinne ambavyo havitakuwa mbinguni. (vyovyote vinne)

    - Dhambi
    - Uchungu
    - Huzuni
    - Migogoro
    - Hatari
    - Ugonjwa
    - Kuzeeka
    - Kifo

3. Je, ni nani ataenda mbinguni?

    Wale watakaotubu dhambi na kumwamini Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana

4. Je, waumini huenda mbinguni wakati gani?

    Wakati wa kifo au wakati Yesu atakaporudi

5. Je, ni mambo gani matatu ambayo Biblia inatuambia kuhusu jehanamu?

    - Ni ya milele.
    - Haiwezi kutenguliwa.
    - Ni mahali pa uchungu mwingi.

6. Je, Yesu alimaanisha nini aliposema mtu anapaswa kukata mkono wake? (Mathayo 5:30).

    Aache kufanya lolote linalomwongoza katika dhambi na jehanamu.

7. Orodhesha sababu tatu kwa nini jehanamu ni ya milele.

    - Dhambi ni kosa dhidi ya Mungu asiye na kikomo.
    - Wenye dhambi humnyima Mungu utumishi wa milele wanaohitaji kumpa.
    - Sisi ni viumbe wa milele na hatuna mahali pengine pa kwenda ikiwa tutachagua kutengwa na Mungu.

# SOMO LA 14

## MATUKIO YA MWISHO

1. Je, ni zipi kweli nne muhimu zilizotolewa katika unabii wa Biblia kuhusu matukio ya mwisho?

    - Kurudi kwa Yesu kimwili
    - Ufufuo wa kimwili wa watu wote
    - Hukumu
    - Ufalme wa milele wa Mungu

2. Je, nini kitatokea kwa Wakristo Yesu atakaporudi?

    - Wale waliokufa watafufuliwa.
    - Wakristo wote watanyakuliwa juu kukutana na Bwana.

3. Je, tunapaswa kusubirije ujio wa Yesu?

    - Kudumisha vipaumbele vya milele
    - Kuishi maisha safi
    - Kujilinda kiroho kwa maombi

4. Je, kwa nini kanuni ya ufufuo ni muhimu?

    - Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.
    - Watu wote watafufuliwa.
    - Mwili una thamani ya milele.
    - Injili ni kweli.

5. Tunapaswa kujua kuhusu hukumu ili tuelewe mambo gani manne?

    - Umuhimu wa dhambi
    - Uwajibikaji wetu kwa Mungu
    - Umuhimu wa maamuzi yetu
    - Mwisho wa dhambi zote

# SOMO LA 15

## KANUNI ZA IMANI ZA KALE

**1.** Kanuni ya imani ni nini?

Muhtasari wa kanuni za msingi za Kikristo

**2.** Taja kauli mbili za kikanuni za kwanza kuhusu Yesu.

- Yesu ni Bwana
- Bwana Yesu Kristo

**3.** Je, rejeo la kanuni ya imani ya kwanza katika maandiko ambalo linatoa kauli kadhaa ni lipi?

1 Timotheo 3:16

**4.** Je, kusudi la Kanuni ya Imani ya Mitume lilikuwa lipi?

Kueleza kanuni za mitume

**5.** Je, kusudi la Kanuni ya Imani ya Nisea lilikuwa lipi?

Kulinda kanuni ya uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu

**6.** Je, kusudi la Kanuni ya Imani ya Chalsedonia lilikuwa lipi?

Kulinda kanuni ya umwilisho wa Kristo